**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**




# TAARIFA YA MCHANGO WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI KATIKA MAENDELEO YA TAIFA KWA MWAKA 2022

**Oktoba, 2023**

## YALIYOMO

YALIYOMO ..... i
VIFUPISHO ..... iv
ORODHA YA MAJEDWALI ..... v
ORODHA YA MAUMBO ..... vi
DIBAJI ..... vii
SHUKRANI ..... ix
MSAJILI WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALITAARIFA KWA UFUPI ..... x
SURA YA KWANZA ..... 1
MSINGI, MALENGO NA WALENGWA WA TAARIFA ..... 1
1.1 Utangulizi ..... 1
1.2 Msingi wa Taarifa ..... 2
1.3 Malengo ya Taarifa ..... 3
1.4 Walengwa wa Taarifa ..... 3
1.5 Mawanda ya Uchambuzi ..... 3
1.6 Mbinu Zilizotumika ..... 4
SURA YA PILI ..... 5
URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI ..... 5
2.1 Utangulizi ..... 5
2.2 Mfumo wa Kisheria ..... 5
2.3 Mwongozo wa Uratibu ..... 5
2.4 Mfumo wa Kielektroniki ..... 6
2.5 Mkakati wa Uendelevu wa Mashirika ..... 6
2.6 Mahitaji ya Kisheria na Kikanuni ..... 7
2.7 Uwasilishaji wa Taarifa na Ulipaji wa Ada ..... 8
SURA YA TATU ..... 10
MAPATO, MATUMIZI NA UENDELEVU WA MASHIRIKA ..... 10
3.1 Utangulizi ..... 10

3.2 Mapato ya Mashirika ........ 10

3.3 Matumizi ya Mashirika ........ 12

3.4 Uendelevu wa Mashirika ........ 13

3.5 Mifano ya Nchi Nyingine ........ 15

SURA YA NNE ........ 17
MCHANGO WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI ........ 17
KATIKA MAENDELEO ........ 17
4.1 Utangulizi ........ 17

4.2 Utekelezaji wa Miradi Kisekta ........ 17

4.2.1 Uhifadhi wa Mazingira ........ 19

4.2.2 Sekta ya Afya ........ 19

4.2.3 Ulinzi wa Jamii ........ 21

4.2.4 Uwezeshaji wa Jamii ........ 22

4.2.5 Sekta ya Elimu ........ 23

4.2.6 Sekta ya Kilimo ........ 29

4.2.7 Utawala Bora ........ 31

4.2.8 Sekta ya Maji ........ 32

4.2.9 Haki za Binadamu ........ 35

4.2.10 Masuala ya Kijinsia ........ 35

4.3 Wanufaika wa Miradi ........ 38

4.4 Ajira za Mashirika ........ 41

4.5 Makato ya Mishahara ya Kisheria ........ 43

4.6 Utekelezaji wa Sera za Ndani ........ 43

SURA YA TANO ........ 45
HITIMISHO ........ 45

5.1 Utangulizi .......... 45
5.2 Changamoto .......... 45
5.3 Hatua za Kuchukuliwa .......... 46
REJEA .......... 47

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| CCBRT | Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania |
| CDC | Centre for Disease and Control |
| DANIDA | Danish International Development Agency |
| EU | European Union |
| FCS | Foundation for Civil Society |
| FCDO | Foreign, Commonwealth and Development Office |
| GePG | Government Electronic Payment Gateway |
| JMT | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| GN | Government Notice |
| KOICA | Korean International Cooperation Agency |
| LCAOF | Liz Claiborne & Art Ortenberg Foundation |
| LSF | Legal Service Facility |
| LVIA | Lay Volunteers International Association |
| MKIUMA | Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali |
| MSPH | Mailman School of Public Health |
| NGOs | Non-Governmental Organizations |
| NIDA | National Identification Authority |
| NIS | NGOs Information System |
| NORAD | Norwegian Agency for Development Cooperation |
| SIDA | Swedish International Development Cooperation Agency |
| TFFT | The Foundation For Tomorrow |
| UNICEF | United Nations Children Fund |
| UNDP | United Nations Development Programme |
| UNHCR | United Nations High Commission for Refugees |
| USAID | United States Agency for International Development |
| WWF | World Wildlife Fund |
| WFT | Women Fund Tanzania Trust |
| WEFTA | Water Engineers for the Americas |

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 2.7 Mikataba Iliyoidhinishwa
Jedwali 3.2: Vyanzo vya Fedha
Jedwali 3.3: Matumizi ya Fedha
Jedwali 4.2: Mchanganuo wa Fedha Kisekta
Jedwali 4.3: Wanufaika wa Miradi Kisekta
Jedwali 4.4 Mgawanyo na Idadi ya Waajiriwa

## ORODHA YA MAUMBO

Umbo 1.1 Usajili wa Mashirika
Umbo 3.2 Vyanzo vya Fedha
Umbo 3.3 Matumizi ya Fedha
Umbo 4.2: Asilimia ya Fedha Kisekta
Umbo 4.3A: Asilimia ya Wanufaika kwa Sekta
Umbo 4.3B: Asilimia ya Wanufaika kwa Makundi
Umbo 4.4A: Asilimia ya Waajiriwa na Wanaojitolea
Umbo 4.4B: Mgawanyo wa Ajira kwa Jinsia

# DIBAJI

Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 inaweka msingi wa uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini. Pamoja na mambo mengine, Sera hii ilitoa maana ya Shirika Lisilo la Kiserikali, kuainisha vyombo vya usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuweka utaratibu wa kusajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Sera hii ilipelekea kutungwa kwa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania, ambayo imempa mamlaka Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kusajili na kuratibu shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa upande wa Tanzania Bara.

Kama mnavyofahamu, Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeendelea kukua kwa kasi hasa kuanzia mwaka 2005, ambapo kulikuwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2,110 hadi Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 8,818 kufikia mwezi Desemba 2022. Ni matarajio ya Serikali kupitia Wizara yenye dhamana kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yataendelea kutekeleza shughuli zake kwa kuzingatia misingi ya uwazi na uwajibikaji kama ilivyoainishwa katika Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Kama sehemu ya jitihada mahsusi za kuongeza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeandaa Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2022. Kwa ujumla, taarifa hiyo pamoja na mambo mengine, imeainisha jukumu la uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini, pamoja na kuainisha mchango wa Mashirika hayo katika utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali, ikiwemo za Mazingira, Afya, Ulinzi wa Jamii, Uwezeshaji wa Jamii, Elimu, Kilimo, Utawala Bora, Maji, Haki za Binadamu, Masuala ya Jinsia, Nishati, Miundombinu na Viwanda. Aidha, taarifa hii imeainisha changamoto na hatua za kuchukuliwa katika utatuzi wa changamoto zilizopo.

Aidha, katika kuhakikisha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanaendelea kutoa mchango wake katika maendeleo ya Taifa, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya utendaji kazi, ikiwemo kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuongeza Ramani ya Kidigitali ya Utambuzi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ambayo ni nyenzo muhimu itakayosaidia kutambua mahali yalipo Mashirika, pamoja na miradi na afua zinazotekelezwa na Mashirika hayo. Kwa kuwa Ramani hiyo itatumiwa na wadau kupitia teknolojia rahisi ya kiganjani, itaziwezesha Taasisi za Serikali, Wadau na Jamii kwa ujumla kupata taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa ajli ya upangaji wa mikakati mbalimbali ya maendeleo kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopo, sambamba na kujenga ubia wenye tija na Mashirika hayo.

Kwa kuzingatia umuhimu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali, napenda kutoa wito kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia misingi ya uwazi na uwajibikaji, kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji baina yake na wadau wengine katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo, pamoja na kuhakikisha kunakuwepo na uendelevu wa Mashirika hayo hapa nchini.

Ni matumaini yangu kuwa taarifa hii itakuwa chachu kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wadau wengine kuendelea kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa uwazi. Vilevile, taarifa hii itaongeza ufanisi na tija katika uratibu na usimamizia shughuli za Masharika Yasiyo ya Kiserikali na hatimaye kuongeza utambuzi wa mchango wake kupitia uimarishaji wa mifumo ya kiutendaji, ushirikiano, pamoja na uwasilishaji na ubadilishanaji wa taarifa baina ya Serikali, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sekta Binafsi, Washirika wa Maendeleo na jamii kwa ujumla.

Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe
**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

## SHUKRANI

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inapenda kutoa shukrani za pekee kwa watu wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika mchakato wa uandaaji, uchapishaji na usambazaji wa Kitabu hiki cha Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2022.

Shukrani za dhati ziende kwa aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara (sasa Katibu Mkuu – Wizara ya Afya), Dkt. John Jingu kwa kuhuisha na kusimia mchakato wa uandaaji wa Kitabu hiki. Vilevile, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali chini ya Mwenyekiti wake, Hajjat Mwantumu Bakari Mahiza, kwa usimamizi na uratibu uliotukuka wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa upande wa Tanzania Bara.

Aidha, shukrani zilifikie Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) chini ya Mwenyekiti wake Dkt. Lilian Badi na Katibu Mkuu wake Bw. Revocatus Sono kwa ushirikiano thabiti ambao wamekuwa wakiutoa kwa Wizara katika kuratibu na kusimamia sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini.

Vilevile, shukrani ziende kwa Menejimenti ya Wizara kwa michango yao ya hali na mali iliyowezesha kuboredha fani na maudhui ya Kitabu hiki cha Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2022. Nawashukuru pia kwa maoni mliyoyatoa na kuridhia kwenu kuchapishwa kwa Kitabu hiki ili kiweze kutumiwa sio tu na wadau wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, bali pia na jamii ya Watanzania kwa ujumla.

Aidha, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Timu ya Wataalam iliyopewa jukumu la kuratibu uandaaji wa Kitabu hiki wakiongozwa na Bw. Charles Komba (Mwenyekiti) na Bw. Faki Shaweji (Katibu). Wajumbe wengine walikuwa ni Bi. Jaina Msangi, Bw. Abraham Mushashu, Dkt. Methusela Masanja, Bw. Godfrey Magesse, Bw. Issa

Mtinangi, Bi. Lusubilo Mwangunga, Bw. Erasto Mwingira na Bi. Josephine Mchalange. Ninawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya!

Mwisho, lakini sio kwa umuhimu, napenda kutoa shukrani za kipekee kwa Kampuni ya Speedy Print Limited, Shirika la Tanzania Human Rights Defenders Coalition (THRDC), Shirika la Management and Development for Health (MDH), Shirika la Legal Services Facility (LSF), Shirika la Plan International, pamoja na Shirika la World Renew kwa kufanikisha uchapishaji wa nakala za Kitabu hiki.



Vickness G. Mayao

**MSAJILI WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI**

## TAARIFA KWA UFUPI

Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni kati ya wadau muhimu wa kimkakati katika kukuza maendeleo ya jamii ndani na nje ya Tanzania. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ina jukumu la kusimamia uratibu wa sekta hii kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini.

Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni nyenzo muhimu ya kupima utendaji kazi wa Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika mwaka husika. Taarifa hii imegawanyika katika Sura kuu tano. Sura ya Kwanza, imeelezea kuhusu jukumu la usajili na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa upande wa Tanzania Bara, msingi na malengo ya kuandaliwa kwa taarifa hii, walengwa wa taarifa, pamoja na mawanda na mbinu zilizotumika katika uandaaji wa taarifa hii.

Sura ya Pili imeeleza kuhusu ni uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hususani kwa kubainisha Mfumo wa Kisheria wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Mahitaji ya Kisheria na Kikanuni, pamoja na Uwasilishaji wa Taarifa na Ulipaji wa Ada.

Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa umeelezewa katika Sura ya Tatu na Sura ya Nne, ambapo taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,257 zimechambuliwa zikiwa na jumla ya mapato ya Shilingi **2,249,244,846,280** na matumizi ya Shilingi **2,192,036,989,575**. Uchambuzi unaonesha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yametoa mchango mkubwa katika utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali hususani katika sekta za Mazingira, Afya, Ulinzi wa Jamii, Uwezeshaji wa Jamii, Elimu, Kilimo, Utawala Bora, Maji, Haki za Binadamu, pamoja na Masuala ya Jinsia.

Aidha, kazi na huduma za Mashirika hayo ziliwanufaisha watoto, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Aidha, jumla ya Taasisi **6,316,968** zilinufaika kutokana na huduma za Mashirika. Kwa upande wa ajira, Mashirika yameajiri jumla ya watu **15,479** ambao wengi wao ni Watanzania. Vilevile, uchambuzi unaainisha sampuli ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambayo yana Sera, Kanuni na Miongozo inayosimamia utendaji wa ndani wa Mashirika.

Sura ya Tano ni hitimisho, ambapo inaelezea umuhimu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kuchangia maendeleo ya jamii kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa. Aidha, imeainisha kuwa changamoto kubwa ni uwasilishaji usioridhisha wa taarifa na uelewa mdogo wa matumizi ya mfumo wa Kielektroniki.

Hivyo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yametakiwa kuzingatia Sheria na Miongozo inayosimamia Mashirika hayo na kwamba Wizara itaendelea kuweka mazingira wezeshi na kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuhakikisha kuwa taarifa zao zinawasilishwa kupitia mfumo wa kielektroniki na mchango wao unatambulika.

# SURA YA KWANZA

# MSINGI, MALENGO NA WALENGWA WA TAARIFA

## 1.1 Utangulizi


Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ina jukumu la kusajili na kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.

Aidha, Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 imeweka misingi ya uwazi na uwajibikaji kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pamoja na kuhimiza ubia kati ya Serikali na Mashirika hayo ili kutambua mchango wao kwa jamii. Katika kutekeleza hilo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yametakiwa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa kazi wanazofanya katika kipindi cha robo mwaka na mwaka ili kuwezesha utambuzi wa shughuli zilizotekelezwa pamoja na mchango wake katika maendeleo ya Taifa.

Wizara pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikifanya ufuatiliaji wa shughuli/miradi inayotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Lengo ni kutathmini mchango unaotolewa na Mashirika hayo katika maendeleo ya nchi, tija ya miradi inayotekelezwa kwa jamii kulingana na Sera za Nchi. Aidha, ufuatiliaji unalenga kupima mwenendo wa utekelezaji wa majukumu ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia sekta hii ikiwa ni pamoja na kufahamu mafanikio na changamoto za kiutendaji katika sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini.

Kwa mwaka 2022, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja kusajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Katika kipindi cha Januari – Desemba 2022 jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali **1,420** yamesajiliwa, ikiwemo ngazi ya Kimataifa (**63),** Kitaifa (**1,289),** Mkoa (**41)** na Wilaya (27) na kufikisha jumla ya Mashirika yote yaliyo hai **8,818** hadi Desemba 2022**.**

**Umbo 1.1 Usajili wa Mashirika**




## 1.2 Msingi wa Taarifa

Katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni, kumekuwepo na uhitaji wa taarifa sahihi za mchango wa sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwemo wadau wa Maendeleo, Taasisi za Utafiti, Sekta Binafsi, Vyombo vya Habari na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Aidha, Serikali imekuwa ikihitaji taarifa sahihi kuhusu utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kutambua mchango wake katika pato la taifa na kuwataarifu watunga Sera na wafanya maamuzi. Hivyo, tathmini ya mwaka 2022 ya Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inatoa taarifa ya mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kitakwimu kwa ajili ya Maendeleo ya Taifa na kutambua fursa mbalimbali ili kuboresha sekta.

## 1.3 Malengo ya Taarifa

Lengo kuu la kuandaa taarifa hii ni kutathmini na kupata picha halisi ya mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa kupitia utekelezaji wa kazi za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa kwa kipindi cha mwaka 2022. Malengo Mahsusi ni pamoja na;

a) Kutambua Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyowasilisha taarifa ya utendaji ya mwaka na kuainisha miradi inayotekelezwa pamoja na matumizi ya rasilimali;

b) Kutathmini utelekezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

c) Kutathmini mifano bora ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yenye Sera za ndani;

d) Kubainisha mifano bora ya nchi zinavyoratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; na

e) Kubainisha changamoto katika uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kupendekeza hatua za kuchukuliwa.

## 1.4 Walengwa wa Taarifa

Walengwa wa taarifa hii ni Wizara yenye dhamana na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi, Washirika wa Maendeleo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na jamii kwa ujumla.

## 1.5 Mawanda ya Uchambuzi

Uchambuzi huu unabaianisha mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kisekta, uzingatiaji wa Sheria na Miongozo, mifano bora ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoka nchi nyingine, uzingatiaji wa malengo, mipango, mikakati na vipaumbele vya kitaifa, upatikanaji wa fedha, pamoja na uendelevu wa sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa ujumla. Uchambuzi huu unahusisha jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali **1257**

miongoni mwa hayo Mashirika **238** ya kimataifa na **1019** ya kitaifa kati ya Mashirika **6,635** yaliyopaswa kuwasilisha taarifa za mwaka 2022.

## 1.6 Mbinu Zilizotumika

Kimsingi, taarifa hii imeandaliwa kwa kuchambua taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zilizowasilishwa kwa mwaka 2022 zikiwemo taarifa za mwaka, mikataba ya fedha, mapato na matumizi, ajira na wanufaika wa miradi iliyotekelezwa na maeneo miradi ilipotekelezwa. Aidha, mbinu ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imetumika katika baadhi ya mikoa kama vile Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha na Manyara ili kujiridhisha na utekelezaji wa miradi kwa jamii.

# SURA YA PILI

# URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

## 2.1 Utangulizi

Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unafanyika kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, pamoja na Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001. Sera hiyo imejenga msingi wa uwepo wa mfumo wa kisheria, kanuni, miongozo na taratibu mbalimbali kwa lengo la kuongeza ufanisi katika uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa upande wa Tanzania Bara.

## 2.2 Mfumo wa Kisheria

Kwa upande wa Tanzania Bara, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanasimamiwa na kuratibiwa kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania, pamoja na kanuni zake. Kwa kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana hadhi ya kisheria (legal personality) yanaweza kuingia mikataba, kushtaki au kushtakiwa kwa jina la Shirika kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 18 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56.

Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 31 (a) na (b) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56, Mashirika yanapaswa kuzingatia Sheria mbalimbali kwenye utekelezaji wa majukumu yao, kama vile Sheria za Uhamiaji, Fedha, Kodi na Kazi, pamoja na kuheshimu mila na desturi za watu na jamii wanapotekeleza shughuli zao.

## 2.3 Mwongozo wa Uratibu

Katika kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara iliandaa Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wa mwaka 2020 ambao umeainisha majukumu na wajibu wa kila mdau wa Sekta katika uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara. Mwongozo huu una lengo la kuondoa mgongano wa uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kurahisisha uratibu wa pamoja.

Mwongozo huo unazielekeza Wizara za kisekta pamoja na mambo mengine kuhakikisha zinafanya kazi na shirika lililosajiliwa kwa mujibu wa Sheria, kuboresha mawasiliano na Msajili katika kuratibu Mashirika, kuwezesha Mashirika kutambua fursa na vipaumbele vilivyopo, kusimamia vigezo vya kitaalamu kulinda maslahi ya nchi na kuhakikisha Mashirika yanatekeleza afua zinazoendana na vipaumbele vya nchi.

## 2.4 Mfumo wa Kielektroniki

Katika kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara imeendelea kutumia Mfumo wa Kieletroniki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (nis.jamii.go.tz) ambao umewezesha usajili wa Mashirika Yasiyo Ya Kiserikali, upokeaji wa taarifa za robo na mwaka za Mashirika, uhuishaji wa taarifa mbalimbali za shirika, upokeaji wa mikataba ya fedha na ulipaji wa ada za mwaka. Aidha, mfumo huo umeunganishwa na mifumo mingine kama vile mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Mfumo wa Kielekroniki wa Malipo Serikalini (GePG).

Aidha, wizara inaendelea na uboreshaji wa mfumo huo, kwa kuongeza kipengele cha Ramani ya Kidijitali ya Utambuzi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Ramani hiyo ni nyenzo muhimu itakayosaidia kutambua mahali yalipo Mashirika, miradi na afua zinazotekelezwa. Pia, itatumika na wadau wengi zaidi kupitia teknolojia rahisi ya kiganjani, hivyo kuwezesha Taasisi za Serikali, Wadau na Jamii kupata taarifa za Mashirika kwa ajli ya upangaji wa mikakati mbalimbali kwa maendeleo ya Taifa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopo na kujenga ubia wenye tija na Mashirika hayo.

## 2.5 Mkakati wa Uendelevu wa Mashirika

Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (MKIUMA) 2022/2023 - 2026/2027 ulizinduliwa rasmi Octoba, 2022 wakati wa Jukwaa la mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Lengo kuu la Mkakati huo ni kuwa dira ya kujenga uwezo thabiti wa Mashirika, utengamano wa kifedha, uhimilivu na ukuaji wa kifedha ili kufikia uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, malengo mahsusi ya Mkakati ni;

a) Kuimarika kwa mazingira wezeshi ya ndani yatakayosaidia uendelevu wa muda mrefu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayofanya kazi nchini Tanzania, ifikapo mwaka 2026/27;

b) Kuimarika na kupanuka kwa wigo wa mitindo ya ufadhili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kukidhi mahitaji yake ya ufadhili ifikapo 2026/27; na

c) Kuimarika kwa uwezo wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza dhima zake ifikapo 2026/27.

Hivyo basi, Mkakati huu ni nyezo muhimu inayotumika na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuyawezesha kuandaa mikakati ya ndani ya kuongeza ufanisi na uendelevu wa Mashirika hayo.

## 2.6 Mahitaji ya Kisheria na Kikanuni

Kwa ujumla, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanapaswa kuzingatia mambo yafuatayo: -

a) Kuwasilisha taarifa za robo mwaka kwa mujibu wa Kanuni ya 20 ya Marekebisho ya Kanuni za mwaka 2019 (Tangazo la Serikali Na. 685/2019);

b) Kuwasilisha taarifa za mwaka na taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 29 (1) (a) na (b) ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56;

c) Kuhuisha taarifa za Mashirika, kwa mujibu wa Kifungu cha 33 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56;

d) Kulipa ada ya mwaka kwa mujibu wa Kifungu cha 38 (2) (b) ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56;

e) Kutoa taarifa za wanufaika wa miradi kwa mujibu wa Kanuni ya 13 (a) ya Marekebisho ya Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Tangazo la Serikali, 608/2018;

f) Kutangaza vyanzo vya mapato mara mbili kwa kila mwaka, uwasilishaji wa mikataba ya fedha na kutoa taarifa ya fedha inayozidi kiasi cha shilingi milioni ishirini (Shilingi 20,000,000) kwa mujibu wa Kanuni ya 13 (a) (b) na (c) ya marekebisho ya kanuni ya mwaka 2018 (Tangazo la Serikali Na. 609/2018). na

g) Kuwa na Sera za Ndani, pamoja na Mpango Mkakati wa Uendelevu wa Shirika.

## 2.7 Uwasilishaji wa Taarifa na Ulipaji wa Ada

Katika kipindi cha mwaka 2022, jumla ya Mashirika **1,257** yamewasilisha taarifa za utekelezaji kati ya Mashirika **6,635** yaliyopaswa kuwasilisha sawa na asilimia 19 ya Mashirika yote. Idadi ya Mashirika yaliyowasilisha taarifa imeongezeka kutoka 957 kwa mwaka 2021 hadi 1,257 kwa mwaka 2022 ikiwa ni ongezeko la asilimia 32.

Aidha, jumla ya Mashirika **2945** yamelipa ada za mwaka kati ya Mashirika **6635** sawa na asilimia 44.4 ya Mashirika yaliyopaswa kulipa ada. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, Mashirika mengi yanalipa ada bila kuwasilisha taarifa za utekelezaji hivyo kusababisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mashirika kushindwa kuonesha kwa ukamilifu mchango wa Mashirika katika maendeleo ya Taifa.

Vilevile, katika kipindi cha mwaka 2022 Mashirika **188** yamewasilisha Mikataba/Makubaliano ya fedha za ufadhili wa miradi kwa mujibu wa Marekebisho ya Kanuni, Tangazo la Serikali Na. 609/2018. Jumla ya mikataba/makubaliano **347** yenye kiasi cha shilingi **278,976,601,389** yamewasilishwa, kufanyiwa uchambuzi na kuidhinishiwa kwa lengo la kutekeleza miradi mbalimbali.

**Jedwali 2.7: Mikataba Iliyoidhinishwa**

| Na. | Sekta/Afua | Idadi ya Mikataba | Kiasi cha Fedha |
|---|---|---|---|
| 1. | Mazingira | 31 | 26,115,990,726 |
| 2. | Afya | 61 | 72,823,244,366 |
| 3. | Ulinzi wa Jamii | 20 | 39,926,971,261 |
| 4. | Uwezeshaji wa Jamii | 112 | 57,519,466,222 |
| 5. | Elimu | 50 | 26,834,620,817 |
| 6. | Kilimo | 18 | 29,284,872,762 |
| 7. | Utawala Bora | 17 | 13,180,535,346 |
| 8. | Maji | 6 | 3,062,362,082 |
| 9. | Haki za Binadamu | 10 | 1,470,517,500 |
| 10. | Jinsia | 11 | 4,891,772,774 |
| 11. | Nishati | 10 | 3,502,478,533 |
| 12. | Miundombinu | 1 | 363,769,000 |
| | **Jumla** | **347** | **278,976,601,389** |

# SURA YA TATU

# MAPATO, MATUMIZI NA UENDELEVU WA MASHIRIKA

## 3.1 Utangulizi

Kwa mujibu wa Kifungu cha 29 (1) (a) na (b) ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana wajibu wa kuwasilisha taarifa za mwaka utekelezaji pamoja na taarifa za fedha zilizokaguliwa. Kupitia uchambuzi wa taarifa hizo, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali naweza kubainisha kiwango cha fedha kilichopokelewa na kutumiwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika mwaka husika, pamoja na mikakati mbalimbali ya uednelevu wa Mashirika hayo.


## 3.2 Mapato ya Mashirika

Katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2022, uchambuzi unaonesha kuwa, Mashirika 1,257 yaliyowasilisha taarifa yalipata fedha kiasi cha shilingi **2,249,244,846,280** kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha. Kiasi hicho ni ongezeko la shilingi **1,054,938,393,048** ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia **88.3** ya mapato ya Mashirika ikilinganishwa na mwaka 2021. Kiasi hicho cha mapato ya fedha za Mashirika ni asilimia 5.3 ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023. Mapato ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka husika yameainishwa hapo chini.

**Jedwali 3.2: Vyanzo vya Fedha**

| Na. | Chanzo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Bakaa | 37,183,474,293 |
| 2 | Msamaha wa Kodi | 540,494,949 |
| 3 | Ruzuku | 290,657,498 |
| 4 | Michango ya Wanachama | 29,230,345,424 |
| 5 | Mapato ya Vitega Uchumi | 3,409,596,633 |
| 6 | Malipo ya Huduma | 5,644,541,839 |
| 7 | Michango ya Jamii | 4,209,588,731 |
| 8 | Wafadhili wa Ndani | 18,776,621,886 |
| 9 | Michango kutoka Sekta Binafsi | 7,582,943,635 |
| 10 | Wafadhili wa Nje | 2,142,376,581,392 |
| | **Jumla** | **2,249,244,846,280** |

**Umbo 3.2 Vyanzo vya Fedha**




Taarifa hii ya mapato inaonesha kuwa, asilimia 95.25 ya mapato ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanategemea fedha kutoka kwa wafadhili wa nje. Aidha, michango ya wanachama katika kutekeleza miradi ya kusaidia jamii imeongezeka kutoka asilimia 0.7 kwa mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 1.3 kwa mwaka 2022.

Vilevile, nguvu zaidi inatakiwa kuwekezwa katika kuyawezesha na kuhimiza mashirika kwenye eneo la kuwekeza kwenye miradi ya kujipatia kipato na uingiaji wa ubia kati ya Mashirika na jamii ili vyanzo hivyo viendelee kukua. Aidha, Mashirika yazingatie kuandaa mipango ya uendelevu itakayoyawezesha kuwa na vyanzo vya kudumu katika utekelezaji wa majukumu yao.


## 3.3 Matumizi ya Mashirika

Katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2022 taarifa zinaonesha kuwa, kiasi cha shilingi **2,192,036,989,575** kimetumika kama ilivyoainishwa hapo chini: -

**Jedwali 3.3: Matumizi ya Fedha**

| Na | Aina ya Matumizi | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Miradi | 1,959,334,118,380 |
| 2 | Posho na Mishahara | 177,828,623,637 |
| 3 | Kodi ya Ujuzi (SDL) | 2,278,365,128 |
| 4 | Kodi ya Mishahara (PAYE) | 26,120,782,241 |
| 5 | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) | 25,713,690,118 |
| 6 | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) | 761,410,071 |
| **Jumla** | | **2,192,036,989,575** |

**Umbo 3.3 Matumizi ya Fedha**




Taarifa hii ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2022 inaonesha kuwa asililia 89.4 imetumika katika utekelezaji wa miradi, asilimia 8.1 ulipaji wa posho na mishahara asilimia 1.2 kulipia kodi ya mishahara.

## 3.4 Uendelevu wa Mashirika

Uchambuzi wa taarifa unaonesha kuwa kwa miaka mitatu mfululizo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakitegemea zaidi ufadhili wa nje kama chanzo cha mapato ili kutekeleza shughuli zake na miradi katika jamii.

Kutokana na hilo, Wizara ilishirikiana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupitia Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiseriklai, Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi, pamoja na wadau wengine kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2022/23 - 2026/27 (MKIUMA), ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati wa kilele cha Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali la Mwaka 2021.

Mkakati huo ulizinduliwa rasmi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), wakati wa kilele cha Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali la Mwaka 2022. Mkakati huo unatumika kama dira ya kujenga uwezo thabiti wa Mashirika, utengamano wa kifedha, ustahimilivu na ukuaji wa kifedha ili kufikia uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Kwa mwaka 2022, inaonesha kuwa asilimia 1.3 na 0.8 za mapato ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanatokana na michango ya wanachama na wafadhili wa ndani. Hii inaonesha kuwa, japokuwa asilimia 95.2 ya vyanzo vya Mashirika vinatokana na ufadhili wa nje kuna ongezeko la mapato kutoka vyanzo hivyo viwili ukilinganisha na mwaka 2021.

Aidha, tarehe 20 Machi hadi 06 Aprili, 2023 Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi maalum na Ofisi ya Rais – Tawla za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ilifanya uhakiki na ufuatiliaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 301 katika Mikoa kumi na nane (18) ya Tanzania Bara. Katika zoezi hilo, ilibainika kuwa Mashirika mengi hayana mikakati ya kujiendesha kwa kutumia vyanzo mbadala bila kutegemea fedha ya ufadhili.

Hata hivyo, baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamebainika kubuni mbinu mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha miradi yao inakuwa endelevu. Mathalan, baadhi ya Mashirika yanayoendesha nyumba kwa ajili waraibu wa dawa za kulevya (sober house), wamekuwa wakishirikisha familia za waraibu na kuzitaka kuchangia kiasi fulani cha fedha kama njia mojawapo ya kufanikisha na kuendeleza programu hizo. Aidha, jitihada za ziada zinahitajika kwa kuwa baadhi ya familia zimebainika kuwa na uwezo mdogo wa kuchangia.

Vilevile, baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yameanza kununua viwanja na kujenga ofisi, kumbi za mikutano na nyumba kwa ajili ya waraibu wa dawa za kulevya kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi wa kiutendaji. Mfano wa mikakati hiyo ni ujenzi uliokuwa unandelea Mkoani Morogoro wa jengo la ghorofa tatu la Shirika la PELUM Tanzania, lenye thamani ya Shilingi Milioni 830.



*Pichani ni jengo jipya la Ofisi za Shirika la PELUM Tanzania, ambalo litatumika pia kama sehemu ya kitega uchumi kwa ajili ya kuliingizia Shirika kipato, ikiwa ni sehemu ya mikakati wa uendelevu wa Shirika hilo*

Aidha, Shirika la Kijana Kwanza (Young People First) la Mkoani Kilimanjaro nao wanaendelea na ujenzi wa ofisi yao yenye thamani ya zaidi ya Shilingi Milioni 700. Mashirika mengine yamekuwa yakitafuta vyanzo mbadala vya kufadhili miradi wanayotekeleza kama vile kufanya harambee na kujihusisha na miradi ya kilimo, mifugo na biashara ili kupata fedha ya ziada ya kutekeleza shughuli na kusaidia wanufaika.

Kwa msingi huo, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau katika kuyajengea uwezo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuhakikisha yana vyanzo vingine vya fedha kwa ajili ya uendelevu wa Miradi wanayotekeleza.

### 3.5 Mifano ya Nchi Nyingine

Tanzania ni mojawapo ya nchi za Afrika yenye utaratibu mzuri katika kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Nchi ya Tanzania imekuwa ikifanya marekebisho ya Kisheria na kujenga mifumo madhubuti ya usajili na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, mfano wa mifumo hiyo ni kuwa na mfumo

wa Kielektroniki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NIS) na kuwa na Wasajili wasaidizi katika ngazi za Halmashauri na Mikoa katika kuratibu shughuli za Mashirika kwa niaba ya Msajili. Hatua hizo zimesaidia kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika kufanya shughuli zake.

Katika kanda ya Afrika Mashariki nchi za Tanzania, Kenya na Rwanda, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakisajaliwa na kuratibiwa na Bodi za uratibu ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Pia nchi hizi zina mifumo ya usajili na uratibu kwa njia ya mtandao (online registration systems) ambayo hurahisisha shughuli za usajili na uratibu wa Mashirika hayo.

Majukumu ya bodi za uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanafanana katika nchi hizo. Bodi hizo zina majukumu ya kusajili, kuhakikisha utekelezaji wa sheria, kanuni na miongozo inayosimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kuyajengea uwezo Mashirika, kuandaa taarifa na kuzisambaza, kukuza uwazi na uwajibikaji, pamoja na kushughulikia malalamiko na migogoro inayohusu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Kwa upande mwingine, katika nchi za Uganda, Senegal na Afrika ya Kusini, shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ikiwemo kuandaa majukwaa ya Mashirika huratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kama ilivyo nchini Tanzania. Majukwaa hayo huwaleta pamoja wadau wa Mashirika na kuweza kuimarisha mitandao ya ushirikiano na kupashana taarifa, kukutanisha wafadhili na Mashirika na kujadili fursa na changamoto zinazoikabili sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kutoka na maazimio ya kukabiliana nazo.

# SURA YA NNE

# MCHANGO WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI KATIKA MAENDELEO

## 4.1 Utangulizi

Mwaka 2001, Serikali ilitunga Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika kujiendesha vizuri na kwa ufanisi katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii. Aidha, Sera hiyo imeweka misingi thabiti ya kutambua mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya nchi kama wadau muhimu na kuweka mifumo ya utekelezaji wake kupitia Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 na Kanuni zake.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana wajibu wa kuzingatia Sera, Sheria na Mipango ya Kitaifa inayosimamia sekta/afua za utekelezaji ikiwa ni pamoja na Sera ya Maendeleo ya Jinsia (1992), Sera ya Elimu na Mafunzo (1995), Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996), Sera ya Kilimo na Mifugo (1997), Sera ya Taifa ya Mazingira (1997), Sera ya Taifa ya Maji (2002), Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii (2003), Sera ya Afya (2007), Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (2013) pamoja na nyingine.


## 4.2 Utekelezaji wa Miradi Kisekta

Kwa kipindi cha mwaka 2022, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yametumia kiasi cha shilingi 1,959,334,118,380 kutekeleza jumla ya Miradi 2,412 katika Sekta/Afua za Mazingira, Afya, Ulinzi wa Jamii, Uwezeshaji wa jamii, Elimu, Kilimo, Utawala Bora, Maji, Haki za Binadamu na Jinsia.

### Jedwali 4.2: Mchanganuo wa Fedha Kisekta

| Na. | Sekta/Afua | Kiasi cha Fedha |
|---|---|---|
| 1 | Mazingira | 840,692,610,323 |
| 2 | Afya | 533,202,283,282 |
| 3 | Ulinzi wa Jamii | 308,792,900,550 |
| 4 | Uwezeshaji wa Jamii | 120,585,673,782 |
| 5 | Elimu | 63,340,017,559 |
| 6 | Kilimo | 31,749,778,791 |
| 7 | Utawala Bora | 29,830,943,245 |
| 8 | Maji | 11,071,960,862 |
| 9 | Haki za Binadamu | 8,908,075,988 |
| 10 | Jinsia | 8,541,620,194 |
| 11 | Nishati | 2,257,717,848 |
| 12 | Miundombinu | 351,535,956 |
| 13 | Viwanda | 9,000,000 |
| | **Jumla** | **1,959,334,118,380** |

### Umbo 4.2: Asilimia ya Fedha Kisekta



### 4.2.1 Uhifadhi wa Mazingira

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni washiriki muhimu katika ulinzi, uhifadhi na utunzaji wa Mazingira. Mashirika yalitekeleza shughuli zao kulingana na programu za Mazingira katika ngazi za Taifa, Mikoa, Wilaya na Ngazi ya Jamii. Kwa mwaka 2022, Sekta ya Mazingira imeongoza kwa kuwa na fedha nyingi na imetumia kiasi cha Shilingi **840,692,610,323** sawa na asilimia **43** ya fedha zote zilizotekeleza miradi.

Uchambuzi unaonesha fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika kuwezesha mamlaka za uhifadhi katika kuboresha hifadhi za taifa, kuweka mazingira rafiki na jamii zinazozunguka hifadhi na tafiti mbalimbali. Aidha, fedha zilielekezwa katika masuala ya upandaji miti na uhifadhi wa misitu, utunzaji wa vyanzo vya maji, uhifadhi wa Mazingira, kujengea uwezo jamii katika utunzaji wa Mazingira, uhifadhi wa ndege na wanyama na uhifadhi wa fukwe za bahari, mito na maziwa.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa, katika sekta ya Mazingira wafadhili wakubwa ni PAMS Foundation US, Swiss Development Agency, World Land Trust, WWF Tanzania Country Office, Franklyn and Marshal College, SIDA, USAID, The Nature Conservancy na UNDP.

### 4.2.2 Sekta ya Afya

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana mchango mkubwa kwenye sekta ya afya ambapo baadhi yanaendesha hospitali, vituo vya afya, zahanati na vituo vya mafunzo ya afya. Aidha, Mashirika mengine yanaendelea kufadhili huduma za afya kama vile UKIMWI, kifua kikuu, malaria, tohara, lishe, afya ya mama na mtoto na UVIKO 19.

Kwa mwaka 2022, Sekta ya Afya imetumia kiasi cha Shilingi **533,202,283,282,** sawa na asilimia 27 ya fedha zote zilitumika katika utekelezaji wa miradi. Uchambuzi unaonesha kuwa, fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika kuwezesha masuala ya Sera na utetezi, masuala ya UKIMWI, afya ya jamii na usafi wa mazingira, UVIKO 19, matibabu ya macho na fistula, utoaji wa viungo bandia, afya ya uzazi na maendeleo ya awali ya mtoto, elimu ya afya ya uzazi kwa vijana balehe, bima, miundombinu ya afya, vifaa tiba na chanjo.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa, wafadhili wakubwa wa sekta ya Afya ni USAID, Bill and Melinda Gate, CDC, AMREF, KOICA, SIFF, FCDO, UKAID, GLOBAL FUND, Master Card Foundation na UNICEF.



*Pichani ni majengo ya Kituo cha Afya cha Dareda Kati kilichopo katika Kata ya Dareda Kati Mkoani Manyara. Ujenzi wa Kituo hiki umefadhiliwa na Shirika la Karim Heart of Spirit Organization*

### 4.2.3 Ulinzi wa Jamii

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana mchango mkubwa kwenye jitihada za pamoja katika kuanzisha na kuhamasisha jamii kupitia programu mbalimbali za ulinzi wa jamii hususani za kulinda maslahi na ustawi wa watoto, wazee, wajane, wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na yatima.

Afua katika Sekta ya Ulinzi wa Jamii zilihusisha utekelezaji wa miradi ya uendeshaji wa makao ya watoto, nyumba salama, makazi ya wazee na vituo vya kulelea watoto wadogo mchana.

Kwa mwaka 2022, Sekta ya ulinzi wa jamii imetumia kiasi cha Shilingi **308,792,900,550** sawa na asilimia **16** ya fedha zote zilizotekeleza miradi. Uchambuzi unaonesha kuwa, fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika masuala ya elimu kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu, kutoa huduma za makazi na malezi kwa watoto, kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, kujengea uwezo familia zinazoishi katika mazingira hatarishi na uwezeshaji wa wanawake.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa katika sekta ya ulinzi wa jamii, wafadhili wakubwa ni USAID, Plan International, ABOTT FUND, UNHCR, Worldshare Head Quorter, US Department of State, European Union, WFT, United Kingdom na Comfort Aid.





*Pichani ni Makao ya Watoto yanayomilikiwa na Shrika la Malaika Children katika Manispaa ya Kinondoni Mkoani Dar es salaam na katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga Mkoani Pwani. Watoto wapatao 80 wanaishi katika nyumba nane zilizopo katika Makao hayo*

### 4.2.4 Uwezeshaji wa Jamii

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni moja ya wadau muhimu katika kuiwezesha jamii hususani katika kuunga mkono jitihada za jamii na kuimarisha uwezo wao wa kujitegemea.

Kwa mwaka 2022, Sekta ya uwezeshaji wa jamii imeongoza kwa kuwa na miradi mingi ya utekelezaji (734) na imetumia kiasi cha Shilingi **120,585,673,782** sawa na asilimia sita (**06**) ya fedha zote zilizotekeleza miradi. Hii inatokana na Mashirika mengi kutekeleza miradi ya uwezeshaji jamii hata kama hayana fedha za kutosha.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliwezesha vikundi mbalimbali vikiwemo vya wanawake na vijana kwenye nyanja za ujasiriamali, ujuzi, kilimo, biashara na uwekezaji, kuwajengea uwezo vijana kwenye masuala ya uongozi na elimu ya uraia. Aidha jamii iliwezeshwa kwenye uzalishaji na uongezaji

thamani wa bidhaa, kupatiwa huduma za urekebu, ajira na kuwezesha watu wenye mahitaji maalumu.

Uchambuzi unaonesha kuwa, katika sekta ya Uwezeshaji wa jamii, wafadhili wakubwa ni Living stone Tanzania Trust, European Union, Nature friends Dresden, Foundation for Civil Society, KOICA, USAID, Master Card Foundation, LSF, Global Affairs Canada na Hans Seidel.




*Pichani ni kisima cha maji kilichochimbwa na Shirika la World Share katika Kijiji cha Zinga, Kata ya Mchanga Kichwa B, Wilayani Bagamoyo kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa Kata hiyo kupata maji safi*

### 4.2.5 Sekta ya Elimu

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yametekeleza miradi ya Elimu hususani ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu, ugawaji wa samani, vitabu na mahitaji mengine yanayohusu sekta ya elimu.

Kwa mwaka 2022, Sekta ya Elimu imetumia kiasi cha Shilingi **63,340,017,559** sawa na asilimia tatu (**03)** ya fedha zote zilizotekeleza miradi. Uchambuzi unaonesha kuwa, fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika masuala ya kutoa ufadhili kwa watoto, kampeni ya kuzuia ukatili dhidi ya watoto na programu ya kuwezesha watoto wa kike kubaki shuleni, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule, kuwajengea uwezo walimu na

utoaji wa vifaa kwa ajili ya elimu kama vile vitabu, kompyuta na sare za shule.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa, katika sekta ya elimu, wafadhili wakubwa ni USAID, Konrad Adeneur, NORAD, Simba switzerland, SIDA, KOICA, US Department of State, Room to Read, TFFT USA Glory Vision Corporation in Korea, Compassion International, World Education Fund USA, Global Affairs Canada na German Federal Ministry for Economic Corporation and Development.





*Pichani ni mradi wa Maktaba uliotekelezwa na Shirika la World Serve kwa lengo la kuwahudumia wanafunzi wa shule za Kawe, Mbezi, Jangwani na walio nje ya shule kutumia muda wa ziada kupata mafunzo na kujisomea*





*Pichani ni majengo ya madarasa ya Shule ya Msingi Gajali iliyopo Kata ya Dareda Kati Mkoani Mnayara. Madarasa hayo yamejengwa kwa ufadhili wa Shirika la Karim Heart of Spirit Organization*



*Pichani ni Kiwanja cha Mpira wa Kikapu kilichojengwa kwa ufadhili wa Shirika la World Serve katika Shule ya Sekondari ya Elerai Mkoani Arusha*




*Pichani ni Maabara ya Kisasa iliyojengwa na Shirika la St. Jude Tanzania katika Shule ya St. Jude Mkoani Arusha*









*Pichani ni mabweni yaliyojengwa na Shirika la World Serve katika Shule ya Sekondari Kiromo iliyo Wilayani Bagamoyo ili kuwezesha upatikanaji wa elimu hasa kwa watoto wa eneo hilo. Mabweni hayo yana uwezo wa kuchukua wanafunzi 108*

### 4.2.6 Sekta ya Kilimo

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yametekeleza miradi ya kilimo hususani mafunzo na na kukuza uelewa wa wakulima wadogo, uongezaji wa thamani wa bidhaa, masoko, usambaji wa pembejeo za kilimo, ufugaji na huduma za ugani. Kwa mwaka 2022, Sekta ya Kilimo imetumia kiasi cha Shilingi **31,749,778,791** sawa na asilimia mbili (**02**) ya fedha zote zilizotekeleza miradi.

Uchambuzi unaonesha kuwa, fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika masuala ya kujengea uwezo wakulima na maafisa ugani kuhusu uzalishaji bora na mbegu za kilimo, kuhamasisha mabadiliko ya Sera na Sheria, kufanya tafiti, kilimo cha misitu, kuongeza thamani kwenye mazao na masoko ya bidhaa za kilimo, namna bora ya kutunza chakula, kukuza uelewa juu ya mabadiliko ya tabia nchi na ufugaji bora wa wanyama.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa, katika sekta ya kilimo wafadhili wakubwa ni VI Agro Forestry, EU, Helvetas, Italian Agency Corporation and Developments, Bill and Melinda Gates Foundation, USAID, Bread for the

World, International livestock Institute, Laudes Foundation na Directorate General for Development Cooperative and Humanitarian Aid (DGD).



*Pichani ni shamba la vitunguu la Kikundi cha Umoja kilichopo Kata ya Ilkidinga Mkoani Arusha. Kikundi hicho kimewezeshwa na Shirika la TRIAS Tanzania*





*Pichani ni baadhi ya miradi ya kilimo cha umwagiliaji cha mboga-mboga Iliyofadhiliwa na Shirika la World Serve katika Shule ya Msingi Burka Mkoani Arusha*

### 4.2.7 Utawala Bora

Kwa mujibu wa mpango kazi wa Taifa wa Utawala Bora, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana mchango mkubwa katika kushawishi mabadiliko ya Sera na utekelezaji wa programu na mikakati ya kukuza utawala bora. Mashirika hayo yanatekeleza shughuli za elimu ya uraia pamoja na kuhimiza masuala ya Sheria, haki za binadamu, uadilifu, uwazi na uwajibikaji.

Kwa mwaka 2022, sekta ya utawala bora imetumia kiasi cha Shilingi **29,830,943,245** sawa na asilimia **1.5** ya fedha zote zilizotekeleza miradi. Uchambuzi unaonesha kuwa, fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika masuala ya usimamizi endelevu wa rasilimali, mafunzo kuhusu elimu ya uraia, usaidizi wa masuala ya sheria kwa makundi mbalimbali, kujengea uwezo vijana na wanawake kuhusu uongozi, haki na uchumi.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa, katika sekta ya Utawala Bora, wafadhili wakubwa ni USAID, Foundation for Civil Society, LCAOF, United State Agency for International Development, Konrad Adeneur Stiftung, Fredrick

Neuman Howlet Foundation, Embassy of Sweden, Norway, Ireland na Denmark, Danida na EU.

### 4.2.8 Sekta ya Maji

Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maji (2002), mpango wa maendeleo na usimamizi wa usambazaji wa maji vijijini unahitaji mahusiano ya kitaasisi kati ya wadau muhimu ambao ni Serikali, Sekta binafsi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na jamii husika.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamehusika katika kutoa mchango kwa jamii katika upangaji, ubunifu, ujenzi na usambazaji wa vifaa, bidhaa na vipuri vinavyohusiana na miradi ya maji nchini hususani maeneo ya vijijini.

Kwa mwaka 2022, Sekta ya Maji imetumia kiasi cha Shilingi **11,071,960,862** sawa na asilimia **0.6** ya fedha zote zilizotekeleza miradi. Uchambuzi unaonesha kuwa, fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika masuala ya elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni na kwenye jamii, uchimbaji wa visima vya maji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji, mafunzo kwa kamati za jamii na jamii, na uboreshaji wa huduma za maji.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa, katika sekta ya maji, wafadhili wakubwa ni Life water International, Play smaktir Hayat derrigi, ComfortAid International, UNICEF, WorldServe International, UNICEF, Charity water, WEFTA na LVIA Italy.





*Pichani ni mradi wa maji safi mashuleni uliotekelezwa katika Shule ya Msingi Zinga kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi wa shule hiyo kupata maji safi na salama wawapo shuleni*



*Pichani ni mabomba ya maji yaliyojengwa kwa ufadhili wa Shirika la Karim Heart of Spirit Organization katika Kata ya Arri Mkoani Manyara*

### 4.2.9 Haki za Binadamu

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yalichangia katika kuendeleza na kuimarisha mfumo wa haki za binadamu nchini. Hii inahusisha ulinzi wa haki za binadamu, mahitaji ya makundi mbalimbali kama vile wanawake, watoto, watu wenye ulemavu, wazee na watu wenye maambukizi ya UKIMWI.

Kwa mwaka 2022, Sekta ya haki za binadamu imetumia kiasi cha Shilingi **8,908,075,988** sawa na asilimia **0.5** ya fedha zote zilizotekeleza miradi. Uchambuzi unaonesha kuwa, fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika masuala ya utoaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi, kampeni za kupinga ukatili wa kijinsia, kuwajengea uwezo na kutoa mafunzo ya kiuchumi na kisheria kwa makundi mbalimbali, kuelimisha kuhusu utoaji wa haki za kijamii na kiuchumi kwa wanawake na wasiojiweza, kujenga uwezo kwa taasisi zinazotoa huduma ya msaada wa kisheria kwa jamii na kutoa elimu ya utetezi na ushawishi kuhusu masuala ya haki za binadamu.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa, katika sekta ya haki za binadamu, wafadhili wakubwa ni Foundation for Civil Society (FCS), International Work Group for Indegionus Affares, Legal Service Facility (LSF) na Oxfarm GB.

### 4.2.10 Masuala ya Kijinsia

Kwa kuzingatia Sera ya Maendeleo ya Usawa wa Kijinsia (2002), Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana wajibu wa kukuza uelewa wa jamii kupitia uhamasishaji, utoaji elimu na kuijengea uwezo jamii, utoaji wa huduma za kijamii na uzingatiaji wa masuala ya jinsia na mafunzo.

Kwa mwaka 2022, Sekta ya jinsia imetumia kiasi cha Shilingi **8,541,620,194** sawa na asilimia **0.4** ya fedha zote zilizotekeleza miradi. Uchambuzi unaonesha kuwa, fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika masuala ya elimu na kampeni za kupinga ukatili wa kijinsia, kuwajengea uwezo wanawake kijamii na kiuchumi, kuwezesha watoto wa kike kubaki shuleni, kuelimisha na kuwezesha watoto wa kike katika masuala ya hedhi salama, kuwezesha wanawake juu ya masuala ya umiliki ardhi na mali.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa, katika Sekta ya Jinsia, wafadhili wakubwa ni UNFPA, USAID, FCDO, UNDP, Bread for the World, Government of Canada-Global Affairs, Children Rights and Violence Prevention Funds.



*Pichani ni Bweni la Wasichana lililojengwa na Shirika la Sawa Wanawake Tanzania katika Shule ya Sekondari Wami iliyopo Mkoani Morogoro. Bweni hilo linawezesha wasichana waliotoka katika mazingira magumu kupata malazi elimu katika mazingira*





*Pichani ni nyumba za walimu na majengo ya vyoo yaliyojengwa na Shirika la Sawa Wanawake Tanzania katika Shule ya Msingi Wami iliyopo Mkoani Morogoro. Mradi huo umewezesha upatikanaji wa makazi kwa walimu na huduma bora za vyoo kwa walimu na wanafunzi wa shule hiyo.*


## 4.3 Wanufaika wa Miradi

Miradi iliyotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika mwaka 2022, imenufaisha makundi mbalimbali katika jamii na taasisi. Unufaikaji huo wa miradi umebainika katika maeneo ya elimu, ujasiriamali, matibabu, kupatiwa zana za utendaji, mitaji na kujengewa uwezo. Wanufaika wa miradi ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali hapa chini:


## Jedwali 4.3: Wanufaika wa Miradi Kisekta

| Na | Sekta | Wanawake | Watoto | Wanaume | Wazee | Wajane | Vijana | Watu Wenye Ulemavu | Jumla ya Wanufaika Kisekta | Jumla ya Taasisi Zilizonufaika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Afya | 1,264,8497 | 51,244,800 | 251,111 | 1,505,056 | 0 | 173,78885 | 4,190 | 83,032,539 | 4,970,526 |
| 2 | Uwezeshaji wa Jamii | 2,550,513 | 314,786 | 431,711 | 115,142 | 796 | 8,481,387 | 3,080 | 11,897,415 | 414,784 |
| 3 | Ulinzi wa jamii | 527,565 | 375,053 | 295,867 | 1,192,479 | 24,339 | 73,399 | 2,502 | 2,491,204 | 755,094 |
| 4 | Mazingira | 743,123 | 418,791 | 623,069 | 586,277 | 0 | 500,995 | 65 | 2,872,320 | 9,604 |
| 5 | Kilimo | 501,190 | 3,453 | 1,106,027 | 1,268 | 82 | 94,983 | 57 | 1,707,060 | 4,639 |
| 6 | Elimu | 124,513 | 507,136 | 9,204 | 0 | 0 | 3,052,505 | 952 | 3,694,310 | 9,592 |
| 7 | Utawala Bora | 4,414,515 | 2,589 | 3,208,460 | 0 | 0 | 1,002,208 | 35 | 8,627,807 | 1,166 |
| 8 | Maji | 390,148 | 48,983 | 15,077 | 33,497 | 0 | 32 | 0 | 487,737 | 113,618 |
| 9 | Haki za Binadamu | 1,408,782 | 32,066 | 146,559 | 0 | 0 | 12,116 | 69 | 1,599,592 | 37,922 |
| 10 | Jinsia | 3,098,491 | 86,176 | 38,887 | 5 | 0 | 65,981 | 0 | 3,289,540 | 23 |
| **Jumla** | | **26,407,337** | **53,033,833** | **6,125,972** | **3,433,724** | **25,217** | **30,662,491** | **10,950** | **119,699,524** | **6,316,968** |

## Umbo 4.3A: Asilimia ya Wanufaika kwa Sekta




## Umbo 4.3B: Asilimia ya Wanufaika kwa Makundi



Uchambuzi unaonesha kuwa, sekta ya afya imeongoza kwa kufikia wanufaika kwa asilimia 69, ikifuatiwa na uwezeshaji wa jamii (10%) na utawala bora (07%). Pia, uchambuzi unaonesha kuwa, Wanawake ndio wanaoongoza kwa kunufaika na miradi ya Mashirika sawa na asilimia 39.27, wakifuatiwa na Watoto ambao ni asilimia 33.49. Wanawake na Watoto wameongoza kwa kuwa miradi mingi hususani ile ya afya na uwezeshaji wa jamii imewalenga wao. Kutokana na uchambuzi, kundi lenye wanufaika wachache ni la watu wenye ulemavu. Vilevile, jumla ya taasisi 6,317,420 zikiwemo vijiji, shule, zahanati, vituo vya afya na hospitali zimenufaika.

Aidha, jumla ya wanufaika wa miradi yote ni 119,699,524, idadi ambayo inazidi jumla ya watanzania waliopo (milioni 61). Hii inatokana na ukweli kwamba, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanajihusha na utekelezaji wa miradi inayogusa sekta/afua mbalimbali ambazo zinailenga jamii hiyohiyo. Hali hii, inapelekea idadi ya wanufaika kuonekana ni kubwa kuliko watanzania waliopo. Aidha, baadhi ya miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inahudumia jamii ambayo sio watanzania kama vile wakimbizi.


## 4.4 Ajira za Mashirika

Kwa mwaka 2022 Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,257 yametoa jumla ya ajira 15,479 kwa makundi mbalimbali ikiwa na waajiriwa 9974 (watanzania 9818 na wageni 156) na wanaojitolea 5505 (watanzania 5255 na wageni 250). Kati ya ajira hizo jumla ya ajira 8627 zilikuwa za wanawake na 6852 zilikuwa za wanaume. Aidha, jumla ya shilingi 177,918,473,876 zimetumika kulipa mishahara na posho za waajiriwa.


**Jedwali 4.4 Mgawanyo na Idadi ya Waajiriwa**

| Na. | Kundi | Watanzania walioajiriwa | Wageni walioajiriwa | Watanzania wanaojitolea | Wageni wanaojitolea | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Vijana | 5,272 | 67 | 3,776 | 136 | 9,251 |
| **2** | Watu Wazima | 4,396 | 86 | 1,334 | 104 | 5,920 |
| **3** | Wazee | 150 | 3 | 145 | 10 | 308 |
| | **Jumla** | **9818** | **156** | **5255** | **250** | **15479** |

**Umbo 4.4A: Asilimia ya Waajiriwa na Wanaojitolea**




**Umbo 4.4B: Mgawanyo wa Ajira kwa Jinsia**



Uchambuzi unaonesha kuwa, Mashirika 10 yanayoongoza kwa kutoa ajira nyingi ni World Vision Tanzania (482), Tanzania Health Promotion Support (THPS) (432), Comprehensive Community Based Rehabilitation In Tanzania (CCBRT) (407), HJF Medical Research International,Inc. (HJFMRI) (338), Amref Health Africa – Tanzania (330), African Relief Organization (238), Plan International (210), Danish Refugees Council (191), BAKAID Tanzania (187) na MSPH Tanzania LLC (168).

### 4.5 Makato ya Mishahara ya Kisheria

Kwa mwaka 2022 Mashirika Yasiyo ya Kiserikali **149** yamechangia kiasi cha shilingi **26,120,782,241** katika Kodi ya Mishahara (PAYE), Mashirika **176** yamechangia kiasi cha shilingi **25,713,690,118** katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mashirika **99** yamechangia kiasi cha shilingi **2,278,365,128** katika Kodi ya Ujuzi (SDL) na Mashirika **158** yamechangia kiasi cha shilingi **761,410,071** katika Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Katika uchangiaji huo, Mashirika yaliyofanya vizuri ni AMREF Health Africa, Foundation for African Medicine Education, Tanzania Health Promotion Support, Plan International, Elizabeth Glaser Pediatric Aids Foundation, Compassion International Inc., Twaweza East Africa, The Jane Goodall Institute Tanzania, Pathfinder International na Danish Refugees Council (DRC).

### 4.6 Utekelezaji wa Sera za Ndani

Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001) inaweka misingi ya uwazi na uwajibikaji ambapo pamoja na mambo mengine inahimiza kuwa na Sera na Kanuni za Ndani ili kuimarisha mifumo ya uwazi na uwajibikaji.

Uwepo wa Sera na Kanuni za ndani za uendeshaji umeelekezwa katika Kanuni ya 14 ya Kanuni Na. 609 ya mwaka 2018 na Kanuni ya 6 (1) (e) ya Kanuni Na. 363 ya mwaka 2008 ili kuhakikisha suala la uwazi na uwajibikaji linazingatiwa, kuepuka mwingiliano wa kimaslahi na kuhakikisha uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Sera na Kanuni hizo ni pamoja na Sera

ya Ajira, Sera ya Fedha, Sera ya Manunuzi, Sera ya Jinsia, Mipango na Mikakati ya muda mrefu, wa kati na mfupi.

Uchambuzi unaonesha kuwa, katika sampuli ya Mashirika 24 yaliyofanyiwa ufuatiliaji Mashirika 18 yalibainika kuwa na Sera na Kanuni za Ndani za uendeshaji sawa asilimia 75 ya Mashirika hayo.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5.1 Utangulizi

Serikali ya Tanzania inatambua kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni mdau mkubwa wa maendeleo nchini. Aidha, inatambua kuwa Mashirika yanafanya kazi kubwa ya kujenga uwezo kwa wananchi hasa katika kutambua haki na wajibu katika kujiletea maendeleo kiuchumi na kijamii. Pia, inatambua kuwa kazi kubwa ya Serikali ni kujenga mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuweza kufanya kazi vizuri, kwa kufuata Sheria na Taratibu zilizowekwa.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kama mdau wa maendeleo wa taifa yameendelea kutoa mchango mkubwa ambao unaonekana kupitia ajira na utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali katika sekta za Afya, kilimo, uwezeshaji wa jamii kiuchumi, Elimu, Mazingira, haki za binadamu, utawala bora na Jinsia.

Kwa mwaka 2022, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamefanikiwa kuwa na kiwango kikubwa cha fedha za utekelezaji wa miradi na kufanikisha kufikia wanufaika wengi zaidi.

## 5.2 Changamoto

Kufuatia uchambuzi wa taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka 2022, changamoto zifuatazo zilijitokeza:-

a) Baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutowasilisha taarifa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni. Kwa mwaka 2022, jumla ya Mashirika 5,378 kati ya Mashirika 6,635 hayakuwasilisha taarifa kwa mujibu wa Sheria. Kutowasilisha taarifa hizo kunapunguza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa.

b) Baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kushindwa kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

(nis.jami.go.tz) kwa usahihi na hivyo kuwasilisha taarifa ambazo hazijakamilika, hali ambayo inapelekea kushindwa kupata taarifa sahihi za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na hatimaye kushindwa kabisa kutambua mchango wa Mashirika husika.

## 5.3 Hatua za Kuchukuliwa

Katika kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kutatua changamoto zinazoikabili Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inatarajia kufanya yafuatayo:-

a) Kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ikiwa ni pamoja na kuendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya Mashirika hayo na kutoa elimu juu ya Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

b) Kuendelea kuhuisha rejista ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuhakikisha Mashirika ambayo hayafuati vigezo na masharti ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania, yanaondolewa kwa mujibu wa Sheria.

c) Kujengea uwezo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wadau mbalimbali namna bora ya kuutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (nis.jami.go.tz) ili kuweza kupata taarifa sahihi na hatimaye kuomngeza utambuzi wa mchango wa Mashirika hayo kwenye jamii.

## REJEA


JMT 1996. Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Jamii, 1996. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

JMT 1999. Mkakati wa Kitaifa wa Utawala Bora, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Kitengo cha Uratibu.

JMT 2022. Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2022/2023 - 2026/2027 (MKIUMA).

JMT 2001. Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, 2001.

JMT 2002. Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali,Sura ya 56 ya mwaka 2002.

JMT 2002. Sera ya Taifa ya Usawa wa Jinsia na Maendeleo ya Wanawake, 2002. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

JMT 2013. Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu, 2013-2017, Wizara ya Katiba na Sheria.

JMT 2004. Kanuni ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Tangazo la Serikali Na. 152, 2004.

JMT 2020. Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara, 2020.

JMT 1977. Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, 1977.



## Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

**Mji wa Serikali - Mtumba,**
**Barabara ya Afya,**
**S. L. P 573,**
**40478 DODOMA.**
**Simu Na: 255-26-2963341/2963346**
**Nukushi: 255-26-2963348**
**Barua Pepe: ps@jamii.go.tz**
**Tovuti: www.jamii.go.tz**